*Mwongozo Na. 1 2016/17*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI VIJIJINI KATIKA AWAMU YA PILI YA PROGRAMU NDOGO YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (WSDP II)

**Desemba, 2016**

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI VIJIJINI KATIKA AWAMU YA PILI YA PROGRAMU NDOGO YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (WSDP II)

## 1.0 UTANGULIZI

Maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yoyote yanategemea rasilimali maji kama nguzo muhimu katika kufikia malengo yaliyowekwa. Upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha una mchango mkubwa katika kuboresha maisha ya jamii husika na kusaidia katika ukuaji wa uchumi. Kama jitihada mojawapo ya kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 *(Tanzania Development Vision - TDV2025),* Serikali imeweka maji katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Awamu ya Pili *(Five Year Development Plan II*) kama kipaumbele kimojawapo katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya viwandani, majumbani, mifugo na utalii.

Tanzania ina kiwango kikubwa cha rasilimali za maji juu na chini ya ardhi. Kiwango cha maji chini ya ardhi kinakadiriwa kuwa kilomita za ujazo **38** na kiwango cha maji juu ya ardhi (*surface water*) kinakadiriwa kuwa kilomita za ujazo **89**, ikijumuisha maji ya Maziwa, mito na chemichemi.

Pamoja na Tanzania kuwa na rasilimali za maji za kutosha, mgawanyo wa rasilimali hizo haupo katika uwiano sawa katika maeneo mengi nchini ambapo kuna uhaba mkubwa wa maji katika maeneo kame. Mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko la watu nchini, ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji, uvuvi na wanyama pori. Vile vile, uharibifu wa mazingira, uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi na matumizi mabaya ya maji husababisha kupungua au kukauka kwa vyanzo vya maji.

Katika kukabiliana na changamoto kwenye utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji na usambazaji maji, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuendeleza na kutunza rasilimali za maji, kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama na kuhimiza matumizi bora ya maji. Juhudi hizo zinafanyika kupitia Sera ya Maji ya Mwaka 2002 ambayo imeweka mfumo madhubuti na endelevu wa kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji nchini. Sera hiyo pia inaelekeza ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya maji katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kubuni, kupanga, kujenga, kusimamia, kuendesha na kuifanyia matengenezo miundombinu ya maji pamoja na kuchangia gharama za huduma za maji. Sera hiyo inatekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2025). Aidha, utekelezaji wa Sera hiyo unasimamiwa kwa Sheria **Na. 11** ya Mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji pamoja na Sheria **Na. 12** ya Mwaka 2009 ya Utoaji wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira.

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji WSDP inatekelezwa kwa kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2006 hadi 2025. Awamu ya Kwanza ya Programuu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (WSDP I) ulianza mwaka 2006/07 na kukamilika mwezi Juni, 2016. Kutokana na baadhi ya miradi kutokukamilika katika awamu ya kwanza, iliamuliwa miradi hiyo iendelee kutekelezwa katika Awamu ya Pili ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (WSDP II), ambayo imeanza kutekelezwa mwezi Julai, 2016 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2019/2020.

## 2.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO

Kama itakavyokumbukwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilikwishatoa Mwongozo kuhusu Utekelezaji Wa Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji mwaka 2007 *(Mwongozo Utekelezaji wa RWSSP Mei 2007-1)* maagizo muhimu katika Mwongozo huu yataendelea kutumika ila kwa yale yaliyofanyiwa mapitio ufafanuzi umetolewa katika Mwongozo huu mpya. Mnasisitizwa kuzingatia maelekezo haya katika utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu WSDP II.

Ufafanuzi katika Mwongozo mpya ni kutoa maelekezo ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini katika Awamu ya Pili ya Programuu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II). Maelekezo haya yamegawanyika katika maeneo Makuu Mawili kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji kwa Halmashauri zote na Sekretarieti za Mikoa – Tanzania Bara. Maeneo hayo ni: -

(i) Masuala muhimu yaliyobainishwa katika utekelezaji wa WSDP I *(Lesson Learnt from WSDP I)*
(ii) Mwongozo Mpya wa Utekelezaji wa Miradi ya maji vijijini kwa Awamu ya pili ya WSDP

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuwawezesha wadau wote muhimu kuelewa malengo na mahitaji ya fedha, utaratibu wa kugawanya fedha, hatua za utekelezaji wa miradi ya maji katika ngazi ya Jamii na Wilaya, utoaji wa taarifa, usimamizi wa miradi ya maji na miongozo itakayotumika katika utekelezaji wa Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

## 3.0 MASUALA MUHIMU YALIYOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA WSDP I *( LESSON LEARNT FROM WSDP I )*

Programuu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji WSDP inatekelezwa kwa kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2006/7 hadi 2025. Aidha, utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programuu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (WSDP I) ulianza mwaka 2006/07 na kukamilika mwezi Juni, 2016. Kutokana na baadhi ya miradi kutokukamilika katika awamu ya kwanza, iliamuliwa miradi hiyo iendelee kutekelezwa katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II), ambayo utekelezwaji wake umeanza mwezi Julai, 2016 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2019/2020.
Katika tathmini iliyofanyika imebainika kuwa Awamu ya Kwanza ya Programuu (WSDP I) imepitia changamoto mbalimbali *(Shortfalls)* ambazo katika Awamu ya Pili ya Programu zimefanyiwa marekebisho ili kuboresha utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI**

Yafuatayo ni mapungufu yaliyobainika *(issues observed)* katika utekelezaji wa Awali ya Kwanza ya WSDP:-

(a) Kukosekana kwa Wakandarasi na Wataalam Washauri wa kutosha wenye sifa na uzoefu katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini. (Baadhi ya usanifu wa miradi uliofanywa haukidhi viwango na ubora unaostahili)

(b) Upatikanaji wa fedha kidogo za utekelezaji wa miradi ya maji na hata zikipatikana hazifiki kwa wakati kwa watekelezaji wa miradi.

(c) Halmashauri kutozishirikisha kikamilifu Sekretarieti za Mikoa katika mapitio ya usanifu wa miradi *(design review)* na usimamizi wa miradi.

(d) Ukosefu wa vifaa/nyenzo za kufanyia kazi. Kwa mfano magari na vitendea kazi katika baadhi ya Ofisi za Sekretarieti za Mkoa na Halmashauri. (Baadhi ya magari yaliyopo katika Halmashauri na Mikoa kutumika kwa kazi nyingine nje ya shughuli za maji.

(e) Kukosekana kwa Wataalam wa kutosha na wenye sifa katika baadhi ya Ofisi za Mkoa na Halmashauri (fani za Uhandisi, Mafundi Sanifu, n.k )

(f) Baadhi ya mapendekezo ya miradi ya vijiji 10 hayakuzingatia kipaumbele cha ujenzi wa miradi katika maeneo yasio na huduma ya maji kabisa. Imeshuhudiwa miradi mipya kujengwa sambamba na miradi ya zamani katika eneo moja.

(g) Timu za Maji za Usafi wa Mazingira za Mkoa na Halmashauri (RWSST na CWSST) hazikutekeleza wajibu wake ipasavyo wa kusimamia utekelezaji wa shughuli za Programu kama ilivyokusudiwa.

(h) Dhana ya utekelezaji wa Miradi ya Vijiji 10 haikueleweka vyema kwa wananchi na kwa watekelezaji mbalimbali wakiwemo Wataalam wa Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa, Wanasiasa na Wadau mbalimbali wa Maji. Wengi walichukulia dhana ya kwamba ni lazima kila Halmashauri iwe na miradi 10 - mradi mmoja kwa kila kijiji, kitu ambacho si sahihi. Matokeo yake ni kulazimisha kutafuta vyanzo vya maji ndani ya kijiji kimoja kimoja, suala ambalo limeongeza gharama za utekelezaji. Hapakuwa na umuhimu wa kufanya hivyo katika maeneo ambayo chanzo kimoja kingeweza kuhudumia kijiji zaidi ya kimoja kwani ni kuongeza gharama za miradi bila sababu za msingi.

(i) Usimamizi mbovu wa Mikataba ya Miradi ya Maji ***(Poor Contract/Project Management)***

- ✓ Miradi mingi kutofanyiwa mapitio ya usanifu *(Design Review*) na usimamizi dhaifu ambao umesababisha miradi kujengwa chini ya viwango na miradi mingine kujengwa kwa gharama kubwa. Aidha, marekebisho katika usanifu wa miradi hiyo umepelekea kuongezeka kwa kazi zaidi.
- ✓ Gharama kubwa za miradi ya maji inayotokana na kutozingatiwa kwa vigezo vilivyowekwa vya kila mradi kutokuzidi gharama ya *per capital cost* ya shilingi 135,000.

Baadhi ya maamuzi yaliyofanyika katika utambuzi wa miradi na miundombinu yake hayakuzingatia ushauri wa kitaalam. Kwa mfano katika mapendekezo ya uchaguzi wa miradi ya vijiji 10, majina ya vijiji vya kipaumbele hayakuzingatia utafiti wa kitaalam. Hali hii ilisababisha miradi mingi kutekelezwa na wananchi kutoonesha ari/nia ya kuhitaji miradi hiyo, suala ambalo limesababisha maeneo mengine yenye shida ya maji kukosa huduma ya maji. Aidha, suala la wananchi kutochangia uendeshaji na matengenezo ya miradi inayotoa huduma

ya maji limebainika kama tatizo maana linakwamisha uendelevu wa miradi na juhudi za Serikali kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma za maji.

(j) Kampeni za usafi wa mazingira hazikuweza kufanyika katika baadhi ya maeneo/vijiji vyenye miradi ya maji

## 4.0 MWONGOZO MPYA WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WSDP II

*(Mwongozo huu ni kwa ajili ya Halmashauri zote na Sekretarieti za Mikoa Tanzania Bara)*

Baada ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programu, Wizara imetayarisha mwongozo huu ili kutoa maelekezo na utaratibu utakaofuatwa katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maji katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Utaratibu ufuatao utafuatwa: -

## 4.1 UKAMILISHAJI WA MIRADI YOTE YA AWAMU YA KWANZA - WSDP (I)

Halmashauri zote zilizosaini Mikataba na Wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyokuwa katika Awamu ya Kwanza (WSDP I) zinaagizwa kukamilisha miradi ya maji iliyopo/iliyokuwepo katika mpango huo kwanza kabla ya kuanza miradi mingine mipya. Kwa hiyo ni wajibu wa kila Halmashauri iliyotekeleza Mpango wa Miradi ya Vijiji 10 kuhakikisha miradi yote iliyoidhinishwa kutekelezwa katika awamu hiyo inakamilishwa.

### 4.1.1 Kwa Miradi inayoendelea

(i) Miradi yote inayoendelea na ujenzi na yenye gharama **chini** ya Shilingi Bilioni 1, na ambayo Wataalam Washauri *(Consultant)* wamemaliza muda wao wa Mkataba *(Time Based Contract)* Sekretarieti za Mikoa inaagizwa kusimamia miradi hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri husika hadi itakapokamilika. Inasisitizwa kuwa kusifanyike Ongezeko la Kazi *(Addendum Work)* kwa Mtaalam Mshauri.

(ii) Miradi yote inayoendelea na ujenzi na yenye gharama **zaidi** ya Shilingi Bilioni 1 iliyofikia/iliyozidi asilimia 50 ya kazi, ambayo Wataalam Washauri *(Consultant)* wamemaliza muda wa Mikataba yao *(Time Based Contract)* Sekretarieti za Mikoa zinaagizwa kusimamia miradi hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri husika hadi itakapokamilika. Inasisitizwa kuwa ili kuepuka gharama zisizo za lazima kusifanyike Ongezeko la Kazi *(Addendum)* kwa Mtaalam Mshauri.

(iii) Miradi inayoendelea na ujenzi na yenye gharama **zaidi** ya Shilingi Bilioni 1 na haijafikia asilimia 50 ya kazi, ambapo Wataalam Washauri *(Consultants)* wamemaliza muda wa Mikataba yao *(Time Based Contract)* Halmashauri husika inashauriwa kufanya mazungumzo *(negotiation)* **mapema** na Mtaalam Mshauri *(Consultant)* kwa ajili ya kuona namna ya kuendelea na kazi hadi itakapofika asilimia 50. Baada ya hapo usimamizi ufanywe na Sekretarieti ya Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri husika. *{ rejea kipengele 4.1.1 (ii) hapo juu}*

(iv) Kwa miradi ambayo haijaanza kutekelezwa, utaratibu wa utekelezaji unatolewa katika ***kipengele 4.1.3*** hapa chini

### 4.1.2 Miradi iliyokuwepo kwenye Mpango wa WSDP I na haikutekelezwa

Kutokana na hali halisi ya miradi inayoendelea ya Vijiji 10 kutotekelezwa yote kwa ujumla wake kutokana na uhaba wa fedha, inasisitizwa kukamilisha viporo vya miradi hiyo ambayo haikutekelezwa kabla ya kuanza miradi mingine. Kwa kuwa miradi iliyotekelezwa ni michache na mingine kuhitajika kukamilishwa kwa kutangazwa, kufanyiwa usanifu au kutafutiwa vyanzo vya maji; utaratibu ufuatao ufuatwe kwa kuzingatia vipaumbele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Miradi iliyosalia na ambayo ilikwishafanyiwa ***usanifu ila haikutangazwa*** kutokana na uhaba wa fedha, basi itangazwe na kuanza kutekelezwa mara moja
b) Miradi iliyopata ***vyanzo vya maji ila haikufanyiwa usanifu*** kutokana na uhaba wa fedha basi ifanyiwe usanifu na kutekelezwa
c) Miradi ambayo ***haikupata vyanzo vya maji***; miradi hiyo ianze kutafutiwa vyanzo vya maji hata nje ya maeneo ya vijiji husika.
Utaratibu wa kutafuta vyanzo vya maji unatakiwa uzingatie ***kipengele 4.1.4 (i)*** hapa chini kinachosema *"Miradi ijengwe kwa kuzingatia vyanzo vya maji vilivyopo/vinavyopatikana na sio kutafuta chanzo cha maji katika kila kijiji. Iwapo chanzo kitapatikana na kuwa na maji ya kutosha, basi kitumike kuhudumia na vijiji vingine vyenye shida ya maji. Vipaumbele (Focus) viwe kwenye vyanzo ambavyo vinaweza kuhudumia vijiji zaidi ya kimoja hasa vyanzo juu ya ardhi ambavyo vina maji mengi (Surface Water, i.e rivers, lakes, dams). Aajiriwe Mtaalam Mshauri/Mkandarasi mmoja kwa ajili ya usanifu na usimamizi wa ujenzi katika vijiji zaidi ya kimoja, kadri iwezekanavyo kuliko kuajiri Mtaalam Mshauri/Mkandarasi kwa kila kijiji.)}"*

### 4.1.3 Utekelezaji wa Miradi Mipya katika Awamu ya Pili ya Programu (WSDP II)

Utekelezaji wa miradi ya maji katika Mpango wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II) umegawanyika katika makundi mawili.

**(a) Miradi ya maji kwa mwaka wa fedha 2016/17**

(i) Halmashauri zote mpya ambazo hazikuwepo katika Mpango Awamu ya Kwanza ya WSDP (I) ziainishe miradi mipya itakayotekelezwa kwa mwaka huu 2016/17 kulingana na bajeti iliyotengwa, ili utekelezaji wa miradi hiyo uanze mara moja. Utekelezaji wa miradi hiyo uzingatie usanifu utakaofanywa na Halmashauri kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mkoa, Ofisi za Mabonde na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zilizopo karibu. Kwa miradi mikubwa Halmashauri zinaweza kuandaa TOR na kuajiri Mtaalam Mshauri kwa kuzingatia taratibu za Manunuzi. Ufafanuzi wa namna ya uibuaji wa miradi mipya kwa Ngazi ya Jamii na Wilaya unatolewa maelezo katika ***kipengele 4.3.3 na 4.3.4***

(ii) Kwa Halmashauri ambazo zinaendelea na utekelezaji wa kukamilisha miradi ya Awamu ya Kwanza ya WSDP (I) zinatakiwa kukamilisha miradi hiyo kwanza kabla ya kuanza miradi mingine. Kutokana na bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2016/17, Halmashauri iangalie kiasi cha fedha kinachosalia baada ya kulipa madeni ya miradi inayoendelea na fedha zilizokwishatumwa kwa mwaka huu 2016/17. Fedha zinazobaki zitumike kutekeleza miradi mipya kwa mwaka 2016/17 kwa utaratibu ulioelezwa katika ***kipengele 4.1.3 (i)***.
*{Miradi hii mipya izingatie kuipa kipaumbele ile iliyosalia wakati wa utekelezaji wa WSDP I* ***(rejea kipengele 4.1.2)***
*Baada ya hapo iwasilishwe Wizarani kwa mapitio na kuwekwa kwenye mpango tayari kwa kutangazwa}*

**(b) Miradi ya maji kwa mwaka wa fedha 2017/18 – 2020/21**

Kila Halmashauri inatakiwa kuaandaa *Council Water Supply and Sanitation Plan (CWSSP)* ya WSDP II kwa miaka minne kuanzia mwaka 2017/18 – 2020/21 na kuwasilishwa Wizarani kwa ajili ya kuingizwa kwenye mpango wa kutafutiwa fedha. Fomati *(Template)* ya ujazaji imeambatishwa. Miradi hii ni pamoja na miradi mipya *(with/without sources & with/without design)*, miradi ya upanuzi na ukarabati *(quickwins projects)*, miradi ya Kimkakati *(Earmarked Projects)*, mabwawa na miradi mingineyo. Ufafanuzi wa namna ya uibuaji wa miradi mipya kwa Ngazi ya Jamii na Wilaya unatolewa maelezo katika ***kipengele 4.3.3 na 4.3.4***

Inasisitizwa kwamba katika maeneo ambayo kuna vyanzo vya uhakika ikiwemo mito mikubwa, maziwa makuu au mabwawa kipaumbele kitolewe kwa miradi inayoweza kuhudumia wananchi wengi na kwa teknolojia ambayo wananchi wataweza kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi hiyo.

### 4.1.4 Maelekezo Muhimu kwa Miradi yote Mipya Itakayojengwa

Maelekezo yafuatayo yazingatiwe wakati wa kutekeleza miradi mipya:-

(i) Miradi ijengwe kwa kuzingatia vyanzo vya maji vilivyopo/vinavyopatikana na sio kutafuta chanzo cha maji katika kila kijiji. Iwapo chanzo kitapatikana na kuwa na maji ya kutosha, basi kitumike kuhudumia na vijiji vingine vyenye shida ya maji. Vipaumbele *(Focus)* viwekwe kwenye vyanzo ambavyo vinaweza kuhudumia vijiji zaidi ya kimoja hasa vyanzo juu ya ardhi ambavyo vina maji mengi *(Surface Water, i.e rivers, lakes, dams)* Aidha, mnashauriwa aajiriwe Mtaalam Mshauri mmoja kwa ajili ya usanifu na usimamizi. Hivyo hivyo, mnashauriwa aajiriwe Mkandarasi mmoja wa ujenzi katika vijiji zaidi ya kimoja, kadri iwezekanavyo kuliko kuajiri Mtaalam Mshauri/Mkandarasi kwa kila kijiji.

(ii) Wananchi/Wakazi waliokaribu na chanzo cha maji na wale ambao makazi yao yanapitiwa na miundombinu mikubwa ya maji wapewe kipaumbele cha kunufaika na upatikanaji wa maji-safi na salama kupitia vyanzo hivyo.

(iii) Mikataba ya utafiti wa maji chini ya Ardhi *(geophysical survey)* na Uchimbaji visima *(exploratory drilling)* ufanyike katika Mkataba mmoja na kwamba atakayetafiti maji

ndiye atakayechimba kisima. Suala la malipo lizingatie upatikanaji wa maji yanayoweza kutumika.

(iv) Vyombo vya Watumia Maji (COWSOs) vinapendekezwa kufanya kazi kulingana na sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Mwongozo wa uundaji na usajili wa COWSO. Ili kuboresha na kuongeza ufanisi COWSO zinaweza kuajiri *Private Operator* (ambaye ataendesha mradi katika masuala ya Kiutawala na Kiufundi *(Management, Financial and Technical).* Aidha, baadhi ya COWSO zinashauriwa kuungana kwa mfumo wa *clustering* ili kuweza kuajiri *Private Operator.* Mwongozo wa utekelezaji wa mfumo huu utatolewa ambapo CWSTs watahusika kuhakikisha utekelezaji wake unafanikiwa na kusaidia masuala yote kwa karibu.

(v) Mapendekezo ya miradi mipya yatoe kipaumbele katika maeneo yasio na miradi/huduma ya maji kabisa. Miradi mipya isijengwa katika maeneo yenye huduma ya maji tayari au yaliyokwishajengewa miundombinu ya maji. Kama mradi unahitaji ukarabati/upanuzi, uainishwe kama mradi wa ukarabati/upanuzi na sio kupendekeza mradi mpya katika eneo hilo.

(vi) Mikataba yote ya Wataalam Washauri *(Consultant)* na Wakandarasi *(Contractors)* iwe katika mfumo wa *Performance Based* na sio *Time Based*

- ♦ Kufanyike *Post Evaluation* ya uhalali *(Due-diligence)* wa Wakandarasi/Wataalam Washauri wanaotegemewa kuajiriwa kabla ya kuwapa kazi.
- ♦ Mikataba isainiwe kwa thamani ya fedha ya Kitanzania (Shilingi ya Tanzania.) ili kuepuka kupanda kwa gharama za miradi ya maji kutokana na mabadiliko ya thamani ya fedha za kigeni *(Cost Inflation).*

(vii) Uhamasishaji kwa kuwatumia Viongozi wa Kisiasa, Serikali za Mkoa na Wilaya ufanyike ili kuhamasisha utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na Wizara kupitia Vingozi na Wataalam mbalimbali pamoja na miongozo yake ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa kuzingatia ubora na viwango.

(viii) Kuhakikisha kampeni za usafi wa mazingira zinafanyika kwenye vijiji vyote ambapo miradi ya maji inataekelezwa.

## 4.2 UTARATIBU UFUATAO UFUATWE KWA AJILI YA KUWATUMIA WATAALAM WASHAURI *(Consultant)* NA WAKANDARASI *(Contractors)* WA MIRADI MIPYA YA MAJI

### 4.2.1 Miradi yenye gharama chini ya Shilingi Milioni 200

Miradi hii itasanifiwa, itajengwa na kusimamiwa na Wataalam wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Ujenzi wa miradi hii utafanywa kwa kuwaajiri mafundi wa kawaida *(Local Fundis)* au kutumia Wakandarasi wadogo *Class 6 & 7* wakishirikiana na mafundi walioajiriwa na Halmashauri.

(i) Usanifu wa miradi hii ufanyiwe mapitio *(design review)* na upate kibali *(No Objection)* kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Msaidizi upande wa Maji *(AAS-Water).*

(ii) Uanzishwaji na Uundwaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji ufanywe na Wataalam wa Ndani *(in-house facilitation).*

(iii) Madai ya Malipo ya Wakandarasi yazingatie kazi iliyofanyika (*deliverables)* na yapitie Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Msaidizi upande wa Maji *(AAS-Water)* kabla ya kufikishwa Wizarani kuombewa fedha.

#### 4.2.2 Miradi yenye gharama kati ya Shilingi Milioni 200 hadi Bilioni 1

Miradi hii itasanifiwa na kusimamiwa na Wataalam wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri, ila ataajiriwa Mkandarasi kwa ajili ya kutekeleza kazi za ujenzi.

(i) Usanifu wa miradi hii ufanyiwe mapitio *(design review)* na upate kibali *(No Objection)* kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Msaidizi upande wa Maji *(AAS-Water)* kisha Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

(ii) Uanzishwaji na Uundwaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji ufanywe na Wataalam wa Ndani *(in-house facilitation).*

(iii) Inasisitizwa kuwa **gharama** za miradi hii ziwekwe kwa ujumla wake zikihusisha kazi nzima/hatua zote za mradi i.e *(Usanifu, Manunuzi ya Wakandarasi na Kazi za Ujenzi)*, kwa maelekezo haya miradi hii isitangazwe katika *LOTs* bali itangazwe na kutekelezwa kwa ujumla wake wa kazi.

#### 4.2.3 Miradi inayozidi Shilingi Bilioni 1

Miradi hii itasanifiwa na kusimamiwa na Wataalam Washauri *(Consultant)* na kujengwa na Wakandarasi *(Contractors)* watakaoajiriwa na Halmashauri husika kwa kuzingatia taratibu za Manunuzi.

(i) Mikataba yote ya Wataalam Washauri *(Consultant)* iwe *Performance Based* na sio *Time Based.*

(ii) Usanifu wa miradi hii ufanyiwe mapitio *(design review)* na upate kibali *(No Objection)* kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

(iii) Uanzishwaji na Uundwaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji ufanywe na Wataalam wa Ndani *(in-house facilitation).*
Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Msaidizi upande wa Maji *(AAS-Water)* ithibitishe kuwa *COWSO* imeundwa na imejengewa uwezo wa kumudu kuendesha na kusimamia miradi.

(iv) Inasisitizwa kuwa **gharama** za miradi hii ziwekwe kwa ujumla wake zikihusisha kazi nzima/hatua zote za mradi i.e *(Usanifu, Manunuzi ya Wandarasi na Kazi za Ujenzi)*, kwa maelekezo haya miradi hii isitangazwe katika *LOTs.* Itangazwe na kutekelezwa kwa ujumla wake wa kazi.

## 4.3 VIAMBATISHO VYA MIONGOZO MINGINE MIDOGO ITAKAYOTUMIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU AWAMU YA PILI – (WSDP II)

Miongozo mingine midogo itakayotumika katika utekelezaji wa WSDO II imeandaliwa, kama ifuatavyo:-

### 4.3.1 Uanzishwaji na Uundwaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji

(i) Miradi yenye gharama chini ya Shilingi **Milioni 200-** Uanzishwaji na Uundwaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji ufanywe na wataalam wa ndani *(in-house facilitation).*

(ii) Miradi yenye gharama kati ya Shilingi **Milioni 200 hadi Bilioni 1 -** Uanzishwaji na Uundwaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji ufanywe na Wataalam wa ndani (in-house facilitation).

(iii) Uanzishwaji na Uundwaji wa Vyombo vya Watumiaji Maji ufanywe na Wataalam wa Ndani *(in-house facilitation).*
Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Msaidizi upande wa Maji *(AAS-Water)* ithibitishe kama *COWSO* imeundwa na imejengewa uwezo wa kumudu kuendesha na kusimamia miradi.

### 4.3.2 Matumizi ya teknolojia mbadala *(renewable energy)*

Kwa kuzingatia kuwa wananchi wengi wanashindwa kuendesha miradi inayoendeshwa kwa kutumia jenereta au injini za dizeli unatolewa wito kwa watekelezaji wa miradi kutumia teknolojia ambazo ni *feasible* kwa masuala ya uendelevu wa miradi ya maji *(Water project sustainability)*. Hatua zifuatazo zifuatwe kuhakikisha uendelevu wa miradi.

(i) Kufuatia mwenendo wa uendeshaji wa miradi ya maji kufanywa na Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs), Halmashauri zinatakiwa kutoa mafunzo ya uelimishaji kwa vyombo hivi ili vielewe umuhimu wa matumizi ya teknolojia mbadala. Katika mafunzo haya wafundishwe ni jinsi gani teknolojia hii itavyopunguza gharama za uendeshaji na matengenezo katika miradi yao hivyo, kuwawezesha kuwa na miradi endelevu na yenye kutoa huduma kwa kipindi kirefu. Uchaguzi wa miradi kwa ngazi ya jamii uhusishe *awareness* ya miradi ya namna hii. Kwa kuzingatia hilo wahakikishe pia wanalinda na kutunza miundombinu yake.

(ii) Wadau/Watekelezaji wa miradi ya maji wahakikishe wanatoa kipaumbele kwa teknolojia mbadala badala ya kuendelea na mfumo wa mazoea wa kutumia teknolojia zenye gharama kubwa hasa kwenye uendeshaji na matengenezo ya miradi hiyo.

(iii) Kwa kuzingatia umuhimu wa teknolojia mbadala, Halamshauri za Wilaya, Miji na Manispaa zitoe kipaumbele kwa miradi ya aina hii, kwa kuzingatia kuwa Wizara inaendelea na juhudi za kuwasiliana na Wafadhili ambao wanaoonesha nia ya kuwekeza kwenye teknolojia hii ikiwa ni pamoja na juhudi za Serikali yenyewe kupitia bajeti yake ya kila mwaka.

### 4.3.3 Hatua za Kufuatwa Wakati wa Kuibua Miradi Mipya katika Ngazi ya Jamii

**Hatua 1: Kutangaza na kuwahamasisha wananchi**

- Kupeleka taarifa kwa wananchi kuhusu kuwepo kwa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira
- Jamii kutambua kuwa maji ni hitaji lao muhimu
- Jamii kuunda Kamati ya Maji na Usafi wa Mazingira na kufungua akaunti
- Jamii kujaza fomu za maombi ya kuingizwa kwenye Programu na kuziwasilisha kwenye Halmashauri

- Kuajiri Wataalam Washauri.

Wahusika ni pamoja na: Jamii, NGOs, DWST, Madiwani,na Wabunge.

**Hatua 2: Uchaguzi wa Awali**

- Kuchambua maombi ya vijiji na kuyapanga kwa kufuata vigezo vilivyokubaliwa. Vigezo hivyo ni pamoja naJamii ionyeshe utayari wa kuchangia sehemu ya gharama za ujenzi na kuendesha mradi wao wa maji.
- Kuunda Kamati ya Maji na Usafi wa Mazingira na kufungua akaunti.
- Jamii ithibitishe kuwa hitaji la maji kwao linapewa kipaumbele.
- Kuwepo kwa magonjwa yanayosababishwa na kutokuwa na maji safi na salama (Kipindipindu, Kuhara damu, Trakoma, n.k.)
- Kutokuwepo kwa migogoro katika jamii husika, n.k.Vijiji vilivyochaguliwa kuarifiwa.Wahusika ni: DWST na Baraza la Madiwani.

**Hatua 3: Kuandaa Mapendekezo ya Mradi**

- Kuiwezesha jamii kuchagua aina ya mradi wanaoutaka na ulio ndani ya uwezo wao wa kuchangia gharama za ujenzi na baadaye uwezo wa kuuendesha.Kutoa mafunzo kwa Kamati ya Maji na usafi wa Mazingira *(WATSAN Committee)* Maandalizi ya awali ya mradi. Wahusika ni: Jamii, CWST, Wawezeshaji na Washauri.

**Hatua 4: Kupitisha Mradi**

- Mradi kupitishwa na kuingizwa kwenye Mpango wa Halmashauri (CWSP).Washauri kusanifu mradi na kuandaa vitabu vya zabuni.Kuteua Mkandarasi na kusaini mkataba/mikataba.Kuendelea na uhamasishaji wa jamii (michango, kujenga uwezo wa Kamati za Maji na Usafi wa Mazingira, n.k.).

Wahusika ni: Jamii, Baraza la Madiwani, DWST, Washauri na Wawezeshaji.

**Hatua 5: Ujenzi wa Mradi**

- Makandarasi kujenga miradi.
- Mshauri kusimamia ujenzi wa miradi.
- CWST kusimamia Washauri, Wawezeshaji na Makandarasi.
- Kujenga uwezo wa jamii kuendesha miradi yao.
- Kusajili vyombo vya uendeshaji vinavyotambulika kisheria.
- Kutoa mafunzo ya uendeshaji.
- Kuhamasisha jamii kuhusu usafi wa mazingira.
- Makandarasi kukabidhi miradi kwa jamii

Wahusika ni pamoja na: Jamii, Wawezeshaji, Washauri, DWST, na Madiwani.

**Hatua 6: Uendeshaji na ufuatiliaji wa Miradi**

Jamii kuendesha miradi yao kupitia vyombo walivyovisajili kisheria. Kufuatilia mwenendo wa uendeshaji, kuandaa taarifa zinazohitajika na kutoa mrishonyuma *(feedback)* kwa jamii. Wahusika ni pamoja na: Jamii, Vyombo vya Watumiaji Maji, Wawezeshaji, CWST, Madiwani, OR-TAMISEMI na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

### 4.3.4 Hatua za Kufuatwa Wakati wa Utangazaji wa Miradi Mipya kwa Ngazi ya Halmashauri

Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji zinasimamia na kushauri wananchi katika kuchagua miradi yao kwa kuzingatia Sera ya Maji ya mwaka 2002. Taratibu zitakazotumiwa na Halmashauri katika kuchagua miradi ya maji zimeainishwa kwenye Mwongozo wa Utekelezaji wa Programu**,** 2006 *(Programme Implementation Manual* – PIM) na Mwongozo wa Kusimamia Utekelezaji wa Programu Ngazi ya Wilaya**,** 2006 *(District Operational Manual - DOM).* Kutokana na miongozo hiyo, Halmashauri zitapitia hatua zifuatazo katika kuchagua miradi:-

**Hatua ya kwanza:**
Kuunda Kamati ya Maji na Usafi wa Mazingira za Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji

**Hatua ya pili:**
Kufanya semina elekezi kwa Wajumbe wa Halmashauri, Uongozi wa Halmashauri na Wadau wengine kuhusu Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

**Hatua ya tatu:**
Kuelimisha jamii kuhusu Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

**Hatua ya nne:**
Kukusanya na kuchambua takwimu za msingi *(baseline data)* za jamii kuhusu Maji na Usafi wa Mazingira

**Hatua ya tano:**
Kutathmini maombi ya jamii kuhusu huduma ya maji na usafi wa mazingira katika vijiji ambavyo miradi yao imepita.

**Hatua ya sita:**
Kutathmini miradi ya jamii ya maji na usafi wa mazingira katika vijiji ambavyo maombi yake yamepitishwa kwenye mchujo.

**Hatua ya saba:**
Kuandaa mpango wa Halmashauri wa maji na usafi wa mazingira kwa kuzingatia miradi ya vijiji vilivyopita kwenye mchujo katika kipindi husika.

## 4.4 Mgawanyo wa Fedha za Utekelezaji wa Miradi ya Maji

### 4.4.1 Mgawanyo katika Sekretarieti za Mikoa

Mgawanyo wa fedha katika Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kufuatilia na kutoa ushauri katika Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini nao umezingatiwa. Mgawanyo utazingatia uwiano wa jumla ya kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya Halmashauri zilizomo ndani ya Mkoa husika pamoja na idadi ya miradi inayotekelezwa.

### 4.4.2 Mgawanyo katika Halmashauri zote/Serikali za Mitaa

Kwa kuwa ipo miradi ya maji inayoendelea na utekelezaji na ipo miradi mipya inatakiwa kuanza kutekelezwa, utoaji wa fedha kwa kila Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji utafanyika kwa kuzingatia makundi ya miradi kama ifuatavyo:-

**(i) Kundi la Kwanza – Miradi inayoendelea na Ujenzi/Miradi yenye madeni**

Pindi Mkandarasi/Mtaalam Mshauri anapomaliza asilimia fulani ya kazi ni wajibu wake kudai malipo ya kiasi cha kazi alizofanya kwa mwajiri wake ambaye ni Halmashauri ili aweze kulipwa. Halmashauri itawajibika kuhakiki malipo hayo kama yanalingana na kazi halisi zilizofanyika *(physical work)* kabla ya kuidhinisha hati za madai yake. Nyaraka/Hati za malipo *(Interim Payment Certificates)* ya kazi zilizofanyika itatakiwa kuwasilishwa Wizarani kwa ajili ya kupitiwa na kuingizwa kwenye orodha ya madeni ya Halmashauri. Endapo itabainika kasoro katika Hati za malipo, Wizara itaiandikia barua Halmashauri namna ya kurekebisha kasoro hizo na kuwasilishwa tena Wizarani, ili ziweze kulipwa.
Fedha zinapopatikana, Wizara itaidhinisha malipo ya madeni halali mapema iwezekanavyo kwa ajili ya kutumwa kwenye Halmashauri husika.

**(ii) Kundi la Pili – Utekelezaji wa Miradi Mipya**

Wizara itatuma fedha za utekelezaji wa miradi mipya kwenda Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kwa kuzingatia vipaumbele vya miradi iliyowasilishwa na Halmashauri Wizarani kupitia CWSSP walizoziandaa. Ni wajibu wa kila Halmashauri kuwasilisha CWSSP kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Awamu ya Pili WSDP, ili waweze kutumiwa fedha hizo kulingana na mahitaji ya miradi husika. Kwa kuzingatia bajeti ya Serikali kwa kila mwaka wa fedha, Wizara itakuwa inatuma fedha za utekelezaji wa miradi hii kulingana na bajeti itakayoidhinishwa na bunge.

Fedha zote za utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira, zitapelekwa moja kwa moja kwenye Serikali za Mitaa kutoka Hazina kwa utaratibu wa "LGCDG System". Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji zitahakikisha kuwa fedha zinatumika kutekeleza Programu kulingana na mipango iliyopitishwa na Halmashauri zao. Ukaguzi wa matumizi ya fedha utafanywa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)* na utafuata taratibu za serikali za ukaguzi wa matumizi ya fedha za umma.

## 4.5 MWISHO

Muongozo huu mpya unaanza kutumika kuanzia tarehe 1.7.2016